Mkulima Mbunifu
Jarida la Kilimo Endelevu Afrika Mashariki
Toleo la 141 | Disemba 2025

## Yaliyomo

Kupima mafanikio ya kilimo kwa mwaka 2
Mbolea za asili huimarisha rutuba 4



Mbolea ya bokashi 5
Bustani za mbogamboga shuleni 6

# Tunapoelekea mwaka mpya 2026; Tuzingatie uhifadhi wa mazingira




***Uhitaji wa ardhi pamoja na malighafi zinazotokana na ardhi unazidi kuongezeka. Ongezeko la watu linamaanisha mahitaji zaidi ya chakula yanahitajika na uzalishaji wa vyakula hivi unategemea ardhi.***

Aidha, malisho kwa wanyama nayo yanahitaji kuzalishwa kupitia ardhi. Hii inamaanisha kwamba sehemu kubwa ya ardhi itatumika kwa kilimo, ili kuongeza eneo la uzalishaji wa mazao, jambo ambalo pia litaongeza uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa vyanzo vya maji na kusababisha mabadiliko zaidi ya tabia nchi.

Ni rai yetu kwa wakulima, wafugaji, wadau mbalimbali katika sekta ya kilimo na ufugaji tujitahidi kuanza mwaka kwa kuweka nguvu katika uhifadhi wa mazingira.

Ungependa kupata jarida la Mkulima Mbunifu? Jarida la Mkulima Mbunifu linachapishwa na kutolewa kwa vikundi vya wakulima bure. Ili kikundi chako kipokee jarida hili basi jaza fomu hii:

**1. Jina la kikundi/taasisi** ..........................................................................

**2. Mahali ulipo** ..........................................................................

**3. Idadi ya wanakikundi: Wanaume** .................. **wanawake** ...................................

**4. Jina la kiongozi** ..........................................................................

**5. Nambari ya simu (rununu)** ..........................................................................

**6. Anuani ya posta** ..........................................................................

**ILANI:** Tafadhali tumia taarifa za fomu hii na uambatanishe majina ya wanakikundi kwenye karatasi tofauti na namba zao za simu. Tuma fomu uliojaza kwa S.L.P 14402, Arusha, Tanzania. Ujumbe Mfupi Pekee: 0785 496036, 0753 96 31 65. Barua pepe info@mkulimambunifu.org.

## *Mpendwa Mkulima*

*Hivi sasa tunaelekea ukingoni mwa mwaka huu wa 2025 na tangu mwaka ulipoanza, katika jarida hili, tumeandika na kuzungumzia mada mbalimbali ambazo tuna hakika kabisa kuwa zimekuwa na faida kubwa katika kukusaidia kuendeleza shughuli zako za kilimo kila siku.*

*Hili linatokana na shuhuda ambazo tumekuwa tukipokea kutoka kwa wakulima, pamoja na kujionea pia yale wanayoyatekeleza shambani.*

*Tangu mwanzo wa mwaka tuliweza kugusia namna kilimo kinavyoweza kutumika kujipatia ajira, umuhimu wa usafi katika shamba na sehemu ya mifugo yako, masoko kwa ajili ya mazao yako pamoja na usindikaji na msisitizo wa matumizi ya taarifa zilizomo katika jarida hili na machapisho mengineyo yanayopatikana katika ofisi zetu.*

*Ni muhimu sana kwa mkulima kujipanga kuanzia sasa ili mwaka unapoanza uweze kufanya shughuli zako kwa ufanisi mkubwa na kujipatia maendeleo bila vikwazo vingi.*

*Hakikisha kuwa unapata taarifa sahihi zinazohusiana na shughuli zako, andaa pembejeo na mahitaji mengine muhimu kama masoko kwa ajili ya mazao ya shamba lako. Kama ni ufugaji basi fuata maelekezo vizuri na ufanye maandalizi thabiti.*

*Niwashukuru wote ambao tumeshirikiana bega kwa bega kwa mwaka wote wa 2025, katika kuhakikisha kuwa wakulima wanapata taarifa sahihi na kwa wakati unaotakiwa. Timu nzima ya jarida la Mkulima Mbunifu inawatakia heri ya sikukuu ya Krismass na sikukuu zote za mwisho wa mwaka, na kheri ya mwaka mpya wa 2026.*

***"Heri ya sikukuu za Christmass na mwaka mpya wa 2026"***

+255 717 266 007
http://www.facebook.com/mkulima_mbunifu
http://twitter.com/mkulima_mbunifu
https://www.instagramu.com/mkulima_mbunifu
mkulimambunifu.org
theorganicfarmer.org
infonet-biovision.org

Wasiliana na *MkM*,
S. L. P 14402, Arusha,
Simu: 0717 266 007, 0762 333 876,
Barua pepe:
info@mkulimambunifu.org
www.mkulimambunifu.org

# Jinsi ya kupima mafanikio ya kilimo mwisho wa mwaka

***Mwisho wa mwaka ni kipindi muhimu kwa mkulima kutathmini safari ya uzalishaji ili kubaini kama malengo yamefikiwa, changamoto zilizojitokeza, na namna ya kuboresha msimu ujao.***

**Erica Rugabandana**

Kutathmini mafanikio ya kilimo siyo tu kuangalia mavuno, bali ni kuchunguza kwa kina gharama, matumizi ya rasilimali, afya ya ardhi, usimamizi wa magonjwa, na mafanikio ya masoko. Tathmini hii husaidia mkulima kufanya maamuzi sahihi, kuepuka makosa ya msimu uliopita, na kuongeza tija.




## 1. Tathmini ya uzalishaji (*Production performance*)

Uzalishaji ni kiini cha shughuli za kilimo. Hapa mkulima anapima:

- Kiasi cha mazao yaliyopatikana kwa ekari/hektari.
- Mabadiliko ya mavuno ukilinganisha na msimu uliopita.
- Ubora wa mazao (daraja A, B, C).
- Upotevu uliotokea shambani au wakati wa uhifadhi.

Mkulima anayefanya tathmini ya uzalishaji hutambua maeneo yaliyofanya vizuri na yale yanayohitaji maboresho ili kuongeza tija.

## 2. Uchambuzi wa gharama na mapato (*Profitability analysis*)

Hili ndilo kipimo muhimu zaidi cha mafanikio. Mkulima anatakiwa:

- Kukusanya rekodi za gharama zote (mbegu, mbolea, dawa, vibarua, matengenezo n.k.).
- Kuweka kumbukumbu za mapato yote kutokana na mauzo.
- Kutengeneza hesabu za faida halisi: Faida = Mapato – Gharama Zote

Ikiwa faida imeongezeka au gharama zimepungua bila kuathiri uzalishaji, mkulima amefanikiwa.

## 3. Malengo ya mwaka na utekelezaji Wake (*Goal achievement*)

Mwaka unaanza na malengo, na mwisho wa mwaka tunatathmini:

- Ni malengo mangapi yametimia (kwa asilimia).
- Ni yapi hayajatimia na sababu zake.
- Ni hatua gani zichukuliwe kuboresha mwaka ujao.

Mfano wa malengo: kuongeza mavuno kwa 30%, kupanua ekari, au kupunguza gharama za dawa.

## 4. Afya ya ardhi (*Soil health review*)

Afya ya udongo huamua uzalishaji wa miaka mingi. Tathmini inahusisha:

- Kupima pH ya udongo.
- Kuangalia upatikanaji wa virutubisho muhimu (NPK, organic matter).
- Kuthibitisha kama rutuba imeongezeka au kupungua kutokana na mbinu za kilimo.

Mabadiliko chanya ya afya ya ardhi ni kiashiria cha mafanikio ya muda mrefu.

## 5. Usimamizi wa wadudu na magonjwa

Mkulima hupima:

- Kiwango cha mashambulizi mwaka huu ukilinganisha na mwaka jana.
- Ufanisi wa mbinu na dawa zilizotumika.
- Gharama zilizotumika kudhibiti changamoto hizi.

Kupungua kwa mashambulizi au gharama zake ni dalili ya usimamizi bora.

## 6. Ufanisi wa matumizi ya rasilimali (*Resource efficiency*)

Hapa mkulima anatathmini jinsi alivyosimamia:

- Maji (umwagiliaji)
- Mbolea
- Nguvu kazi
- Vifaa na mitambo

Rasilimali zikitumika kwa ufanisi, uzalishaji unaongezeka bila kupandisha gharama.

## 7. Mafanikio ya masoko (*Market performance*)

Masoko huamua mapato. Tathmini inahusisha:

- Upatikanaji wa soko la uhakika.
- Mabadiliko ya bei.
- Idadi ya wateja wapya na mikataba mipya.
- Changamoto za soko zilizojitokeza.

## 8. Maendeleo ya miundombinu ya shamba (*Farm infrastructure progress*)

Mkulima huchunguza kama mwaka huu:

- Aliboresha miundombinu (ghala, visima, mabanda, mifereji).
- Ameinua teknolojia ya uzalishaji (umwagiliaji, sensa, vifaa vipya).

*Mkulima Mbunifu* ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaeneza habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika Nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni mojawapo ya mradi wa mawasiliano ya wakulima unaotekelezwa na Biovision (www.biovision.ch) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), (www.kilimo.org), Morogoro. Jarida hili linafadhiliwa na Biovision Foundation

**Wachapishaji:** African Insect Science for Food and Health (ICIPE), S.L.P 30772 – 00100 Nairobi, Kenya, Simu: +254 20 863 2000, icipe@icipe.org, www.icipe.org

**Mpangilio**: Cathbert Msemo 0757 847 481
**Mhariri:** Erica Rugabandana
**Mhariri Msaidizi:** Flora Laanyuni
**Anuani:** *Mkulima Mbunifu*
Sakina, Majengo road, (Elerai Construction Block)
S.L.P 14402, Arusha, Tanzania
Ujumbe mfupi pekee: 0785 496 036, 0766 841 366
Piga simu: 0717 266 007, 0762 333 876
Barua pepe: info@mkulimambunifu.org
www.mkulimambunifu.org

- Ameongeza uwezo wa kuhifadhi au kuchakata mazao.

Miundombinu bora huongeza tija kwa miaka mingi ijayo.

### 9. Ujuzi na mafunzo (*Skills and capacity building*)

Mafanikio ya mkulima yanategemea ujuzi:

- Idadi ya mafunzo aliyohudhuria.
- Maarifa mapya aliyoanza kutumia shambani.
- Ufanisi wa teknolojia mpya alizojaribu.

Kadri mkulima anavyojifunza zaidi, ndivyo maamuzi yake yanavyokuwa bora.

### 10. Changamoto na fursa za mwaka ujao

Mwisho wa mwaka, mkulima huainisha:

- Changamoto kuu alizokutana nazo.
- Sababu za changamoto hizo.
- Fursa alizogundua na jinsi ya kuzitumia mwaka ujao.

## JEDWALI LA KUJITATHMINI MWISHO WA MWAKA (*SELF-ASSESSMENT TOOL*)

| ENEO LA TATHMINI | MAELEZO YA KUTATHMINI | MATOKEO YA MWAKA HUU | MWAKA ULIOPITA | TANZU / TOFAUTI | TATHMINI (ZURI / CHA KUBORESHWA) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Uzalishaji** | Kiasi cha mavuno kwa ekari na ubora wa mazao | | | | |
| **Gharama za uzalishaji** | Gharama zote za mbegu, mbolea, dawa, vibarua, n.k. | | | | |
| **Mapato** | Mapato kutoka mauzo ya mazao yote | | | | |
| **Faida halisi** | Faida = Mapato – Gharama zote | | | | |
| **Malengo ya mwaka** | Asilimia ya malengo yaliyotimia | | | | |
| **Afya ya udongo** | pH, rutuba, virutubisho | | | | |
| **Wadudu/magonjwa** | Kiwango cha mashambulizi na gharama za kudhibiti | | | | |
| **Rasilimali** | Ufanisi wa matumizi ya maji, mbolea, na nguvu kazi | | | | |
| **Masoko** | Upatikanaji wa wateja, bei, na mikataba | | | | |
| **Miundombinu ya shamba** | Maboresho yaliyofanyika mwaka huu | | | | |
| **Mafunzo/ujuzi** | Maarifa mapya uliyojifunza mwaka huu | | | | |
| **Changamoto kuu** | Changamoto ulizokutana nazo | | | | |
| **Fursa mpya** | Fursa zinazoonekana mwaka ujao | | | | |

Kutathmini mafanikio ya kilimo mwisho wa mwaka ni hatua muhimu ya kupanga na kuboresha msimu unaofuata. Kwa kutumia makala hii na jedwali la kujitathmini, mkulima anaweza kupanga mikakati ya kuongeza tija, kupunguza gharama, na kufanikisha kilimo cha kibiashara chenye uhakika wa faida.

# Mbolea za asili huimarisha udongo na kutengeneza rutuba

***Nchini Tanzania, shughuli nyingi za uzalishaji hufanyika katika sekta ya kilimo huku ikiwa imeangazia mazao makuu ya chakula, biashara na mazao ya muda mfupi kama vile mbogamboga.***

**Flora Laanyuni**

Hata hivyo, ili mkulima aweze kuzalisha chakula kingi, bora na salama ni lazima kuhakikisha anazalisha katika udongo wenye rutuba ya kutosha ndipo atakapopata matokeo chanya.

Kwa mantiki hii basi, kulingana na kuwa maeneo mengi ardhi imetumika kwa uzalishaji kwa miaka mingi rutuba imepotea na uzalishaji unakuwa duni, hivyo wakulima sasa hukimbia madukani kununua mbolea kwa ajili ya kuongeza rutuba kwenye udongo na kuzalisha kwa tija.

Aidha, wakulima walio wengi hivi sasa wanalalamika kuwa uzalishaji wa mazao umekuwa ukipungua kila mwaka. Mbali na kutumia vitu vyote vinavyohitajika kama vile mbegu zilizothibitishwa pamoja na mbolea kwa kiasi kinachopendekezwa, bado uzalishaji unakuwa hafifu. Ni vigumu sana kutaja moja kwa moja sababu za hali hiyo.

Watafiti na wanasayansi wanatupa tahadhari! Rutuba katika udongo imekuwa ikipungua kutokana na kulimwa na kutifuliwa mara kwa mara bila kuwa na mikakati dhabiti ya kuulisha udongo. Wakulima wengi hawajui namna ya kukabiliana na jambo hili, na wakati mwingine wanakosa uwezo na vitendea kazi.

Zipo mbinu mbalimbali ambazo mkulima anaweza kutumia kuunda rutuba ya udongo kwa upya.

## Jenga rutuba ya udongo kwa kutumia samadi

Suluhisho la kipekee kwa wakulima ni kurudisha rutuba iliyopotea kwenye udongo. Usemi wa Mkulima Mbunifu ni huu *'Lisha udongo ili ulishe mimea'.* Wakulima wadogo wadogo wana mbinu nyingi za kufanya jambo hili. Samadi, mboji, matandazo pamoja na mkojo wa wanyama ni chanzo kizuri cha virutubisho kwa mazao ya aina yote.

Aina tofauti za samadi kama zile zinazotokana na mchanganyiko wa mkojo wa wanyama na mimea ya asili mfano alizeti mwitu (*tithonia*) imeonesha mafanikio mazuri sana katika kusaidia kukuza mimea. Hii inasaidia kupatikana kwa aina zote za virutubisho vinavyohitajika katika mimea na inaweza kutumika badala ya kutumia madawa na mbolea za viwandani.

Mkulima pia anaweza kutumia mimea iliyovundikwa kama vile, mashona nguo, mwarobaini na mengineyo iliyochanganywa na EM 1 na molasi na kunyunyiza kwenye mimea.



Picha:MkM

## Mbolea vunde

Mbolea vunde inasaidia kuongeza rutuba ya udongo kwa haraka.

Mbolea vunde inatokana na mimea inayokuwa kwa haraka, ambayo hupandwa kwa lengo la kuboresha udongo. Ukipanda mazao mseto kwa kuchanganya mazao jamii ya mikunde kama ya kupanda zao la msimu kama vile kabichi), kabichi itafaidika na kupata virutubisho vya nitrogen, (pia Potassium na Phosphorus) zinazotokana na mimea ya jamii ya mikunde.

## Matandazo

Fyeka mimea jamii ya mikunde na utandaze shambani mwako au acha mabaki ya mimea mara baada ya mavuno yaendelee kufunika udongo lakini pia kuchakatwa na wadudu na kubadilika kuwa mbolea.

## Mazao funika

Otesha mazao funika katika shamba wiki moja kabla ya kupanda kabichi. Mimea inayotambaa huongeza na kushika virutubisho kwenye udongo, kuongeza malighafi zinazooza kwenye udongo, kuzuia madini ya naitraiti kuzama kwenye udongo, virutubisho kutiririshwa, na mmomonyoko wa udongo.

Jambo la muhimu hapa ni kuwa udongo umefunikwa ili kuzuia uharibifu. Mimea jamii ya mikunde inapendekezwa zaidi kwa kuwa husaidia kuongeza nitrojeni kwenye udongo inayopatikana hewani. Inashauriwa pia kuchanganya mimea jamii ya mikunde na nyasi kwa kuwa nyasi hutumia nitrojeni nyingi sana kutoka kwenye udongo, hivyo itasaidia kutokuharibika kwa mtiririko mzima wa uwekaji wa nitrojeni kwenye udongo.

## Mbolea ya fosifeti na mabaki ya mimea

Ukichanganya mbolea ya fosifeti na mabaki ya mimea kama vile mabua ya mahindi na maharagwe kwenye mimea yako itasaidia kutengeneza tindikali ya asili itasaidia na kutengeneza fosiforusi kwa ajili ya mimea yote. Unaweza kutumia mbolea nyingine ya aina hii inayopatikana katika eneo lako kwa kushauriana na wataalamu wa kilimo.



Picha:MkM

# Namna ya kutengeneza mbolea kirutubishi cha udongo

***Kama tunavyofahamu kuwa, bila kulisha udongo rutuba ya kutosha basi ni dhahiri kuwa uzalishaji wowote utakaofanyika katika eneo husika utakuwa hafifu na usiokuwa na tija.***

**Stephano Aminiel**

Tumezungumzia na kuelimisha juu ya uzalishaji wa mbolea za aina nyingi ikiwemo mboji, samadi, chai ya mmea na nyinginezo lakini kwa leo tungependa pia mkulima ajifunze namna ya kutengeneza mbolea aina ya kirutubishi.




## Vifaa na Malighafi zinazotumika:

**Vifaa:** Chombo kilichotengenezwa maalumu kamavile; ndoo au pipa lenye chekecheke ndani na bomba kwa nje na mfuniki usiruhusu hewa kupita/kupenya

**Malighafi:** Malighafi zinazotumika ni pamoja na mabaki ya vyakula, taka za jikoni kama vile maganda ya viazi, maganda ya ndizi na nyanya zilizoharibika, majani na mimea laini, taka za mboga mboga toka sokoni.

## Namna ya kutengeneza mbolea kirutubishi

- Safisha chombo vizuri na kiwe safi
- Katakata au pondaponda malighafi ziwe laini na rahisi kuweka kwenye chombo na kuozesha kwa urahisi.
- Weka malighafi kwenye chombo kwa tabaka za unene wa inchi 4 Hadi 6 kutegemeana na ukubwa na chombo unachotumia kutengenezea mbolea hiyo
- Nyunyiza vimelea chochezi vilivyochanganywa na pumba kwa ujazo wa kiganja cha mkono wa mtu nzima kimoja hadi viwili kwa chombo kidogo (ndoo ya plastiki) na viganja viwili hadi vinne kwa chombo kikubwa (pipa/dramu)
- Endelea kupanga taka nyingine kwa unene uleule na kuendelea kunyunyizia, vimelea chochezi vilivyo changanywa na pumba kwa vipimo na utaratibu huohuo hadi kujaza chombo.
- Funika kwa umakini ili kuhakikisha hewa haipenyi kuingia ndani ya chombo na kuhakikisha bomba/koki imefungwa vizuri na haivujishi.
- Acha mchanganyiko huo ukae kwa muda wa siku isihirini na moja (wiki tatu) kwenye sehemu tulivu yenye kivuli.
- Baada ya siku ishirini na moja fungua bomba na kumimina kirutubishi na kuifadhi kwenye chombo safi mfano chuma ya plastiki yenye mfuniko usioruhusu hewa kupenya ndani
- Mabaki yaliyobaki kwenye chombo yanatumika kutengeneza mbolea ya mboji.

## Namna ya kutumia kirutubishi kwenye mimea.

- Changanywa mbolea ya kirutubishi kwa uwiano wa Lita moja ya kirutubishi kwa Lita mbili za maji ambazo ni sawa na mililita au CC 100 za mbolea ya kirutubishii kwa lita 20 za maji.
- Mbolea ya kirutubishi iwekwe Baada ya kumwagilia mimea na weka kiasi cha CC 15-20 ambayo ni sawa na ujazo wa vifuniko viwili vya chupa ya maji ya Kilimanjaro kwa kila mmea endapo ni zao la mchicha mwagilia mchanganyiko wa maji na mbolea katikati ya mraba ardhini kwa umbali wa futi moja moja.
- Kwa mimea ikiwa bado ni michanga weka maramoja kwa wiki na kwa mimea ambayo imekuwa weka baada ya wiki mbili lengo ni kuharakisha ukuaji na kuepuka mashambulizi ya kasi kwa wadudu pia kusaidia kutibu udongo
- Ili kuhakisha kisambaza mbolea haifikiwi na joto la jua inashauriwa kufukia kwa udongo kiasi

**Muhimu:** Kirutubishi hiki kinafanya kazi ya kuongeza uzalishaji wa vimelea vinavyoozesha taka hai zanazotokana na mimimea (*organic matter*) kwenye udongo na kubadilisha kwa haraka kuwa chakula cha mimea *(humus*) ambayo inafyonzwa na mimea baada ya kuyeyushwa na maji.

## Jinsi ya kutengeneza mbolea ya *supergrow au booster*

Hatua zifuatazo ni muhimu vifaa

- Lita 180 za maji
- Kilo 50 za kinyesi kibichi cha ngo'mbe
- Lita 4 za maziwa
- Lita 4 za molasi
- Lita 4 - 5 za majivu, *phosphates*, au vumbi la miamba
- Gramu 100 - 150 za *yeast*/amira/uyoga

## Hatua za utengenezaji

- Kinyesi kibichi huchanganywa na maji kisha koroga
- Kimininika cha lita 40 hutengenezwa na kutumika.
- Ongeza, maziwa, molasi na majivu na mchanganyiko wa kinyesi cha ngo'mbe
- Kiasi cha lita 40 kilicho tengwa na kuchanganywa kwa muda wa siku 5
- Baada ya siku 5 kiasi cha lita 40 kiongezwe kwenye ndoo kila baada ya siku 4 hadi pale pipa litakapo jaa (lita 180)
- Pipa hufungwa zaidi ili kuruhusu uchachushwaji kuendelea
- Uchachushwaji hufanyika kwa muda siku 30

# Umuhimu wa bustani za mbogamboga za kilimo hai shuleni kwa ajili ya watoto

***Bustani za mbogamboga za kilimo hai mashuleni zimekuwa sehemu muhimu katika kukuza afya, elimu na maendeleo ya watoto. Kwa kuzingatia changamoto za lishe duni, ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza, na hitaji la kukuza mazingira endelevu, shule zimeanza kuwekeza katika bustani za kilimo hai kama njia ya kujifunza na chanzo cha lishe bora.***

**Erica Rugabandana**

Bustani hizi hutoa fursa kwa watoto kujifunza kwa vitendo, kula chakula salama, na kujenga uelewa wa mazingira na uzalishaji wa chakula.

## 1. Kukuza lishe bora na afya ya watoto

Bustani za kilimo hai hutoa mbogamboga safi, salama na zenye virutubisho vingi kama vile vitamini, madini na nyuzinyuzi. Kwa kuongeza mboga kama mchicha, spinachi, matembele, karoti, bamia na nyanya kwenye mlo wa wanafunzi, shule hupunguza hatari ya:

- Utapiamlo
- Upungufu wa damu
- Magonjwa yanayotokana na upungufu wa vitamini na madini

Watoto wanaopata mboga mara kwa mara wanakuwa na afya bora, kinga imara ya mwili na uwezo mzuri wa kujifunza.

## 2. Kujifunza kwa vitendo na kuimarisha elimu

Bustani za shule ni darasa la wazi. Kwa kupitia kilimo hai, watoto hujifunza:

- Misingi ya sayansi ya mimea
- Mzunguko wa maisha ya viumbe
- Umuhimu wa udongo, maji na mwanga
- Ujasilimali kupitia uzalishaji wa mazao
- Stadi za kazi na uwajibikaji

Mtazamo wa "kujifunza kwa kufanya" unasaidia kuongeza uelewa, ubunifu na shauku ya masomo kama sayansi, mazingira na hisabati.

## 3. Kukuza mazingira safi na rafiki kwa afya

Kilimo hai hakitumii kemikali kali kama viuagizo na mbolea za viwandani, hivyo bustani hizi:

- Zinalinda udongo dhidi ya uharibifu
- Zinaongeza viumbe hai kwenye mazingira ya shule
- Zinaimarisha uoto wa asili na kuvutia vipepeo, ndege na wadudu rafiki
- Zinapunguza uchafuzi wa maji na hewa
- Shule zinakuwa na mazingira tulivu, yenye kijani na salama kwa watoto kucheza na kujifunza.

## 4. Kujenga tabia za ulaji wa mboga na afya kwa maisha yote

Watoto wanaoshiriki kupanda, kumwagilia, kuitunza na kuvuna mboga huwa na uwezekano mkubwa wa:

- Kula mboga mara nyingi
- Kupenda vyakula vyenye afya
- Kupunguza ulaji wa vyakula vya mafuta na sukari nyingi
- Uzoefu huu hujenga msingi wa ulaji bora na tabia zinazodumu hadi ukubwani.

## 5. Kuimarisha ari ya ushirikiano na kujenga stadi za kijamii

Bustani za kilimo hai zinahitaji kazi ya pamoja. Kupitia vikundi vya wanafunzi, watoto hujifunza:

- Ushirikiano
- Mawasiliano
- Uwajibikaji







- Uongozi
- Kuamua na kutatua changamoto
- Stadi hizi ni muhimu kwa maisha ya kijamii na kitaaluma ya baadaye.

## 6. Kuchangia uchumi wa shule

Mazao yanayovunwa yanaweza:

- Kutumika kwenye chakula cha wanafunzi
- Kuuzwa ili kuongeza kipato cha shule
- Kusaidia kununua mbegu, vifaa au kuboresha bustani

Hivyo, bustani za shule zinakuwa chanzo endelevu cha rasilimali.

## 7. Elimu ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi

Kupitia bustani za kilimo hai, watoto hujifunza:

- Umuhimu wa kuhifadhi mazingira
- Athari za ukataji miti na uchafuzi
- Mbinu za kudhibiti taka kama kutengeneza mboji (*compost*)
- Matumizi sahihi ya maji na uhifadhi wake
- Uelewa huu unawajenga kuwa wataalam na viongozi wanaojali mazingira kwa vizazi vijavyo.

Bustani za mbogamboga za kilimo hai mashuleni ni zaidi ya chanzo cha chakula. Ni darasa la elimu, msingi wa afya njema, eneo la kukuza ustadi wa kijamii, na hatua ya kujenga kizazi kinachojali mazingira. Shule, wazazi na jamii wanapaswa kushirikiana kuanzisha na kuendeleza bustani hizi ili kuhakikisha watoto wanapata elimu bora, lishe bora na mazingira bora kwa ukuaji wao.

# Umuhimu wa lishe shuleni katika kukuza afya na akili za watoto

***Lishe bora shuleni ni nguzo muhimu katika kukuza afya, ujifunzaji bora na maendeleo ya jumla ya watoto. Wanafunzi hutumia muda mwingi wakiwa shuleni, hivyo mazingira ya shule yana nafasi kubwa katika kuhakikisha watoto wanapata chakula chenye virutubisho sahihi kwa ukuaji na ustawi wao.***

**Flora Laanyuni**

Umuhimu wa lishe shuleni unaweza kuonekana katika maeneo mbalimbali, kuanzia afya ya mwili, maendeleo ya ubongo, tabia na utendaji wa kitaaluma.



Picha:MkM

## 1. Kukuza afya na ukuaji wa mwili

Watoto wako katika hatua muhimu ya ukuaji, na miili yao inahitaji virutubisho kama protini, vitamini, madini, na wanga ili kukua vizuri. Lishe duni inaweza kusababisha utapiamlo, udumavu, upungufu wa damu (*anemia*) na kinga dhaifu ya mwili. Kwa kuhakikisha wanafunzi wanapata chakula bora shuleni, jamii hupunguza hatari ya maradhi yanayotokana na lishe duni na kuwawezesha watoto kukua imara na wenye afya njema.

## 2. Kuboresha uwezo wa kufikiri na utendaji darasani

Ubongo unahitaji nishati na virutubisho sahihi ili kufanya kazi kwa ufanisi. Wanafunzi wanaokula vizuri huonyesha:

- Umakini mkubwa darasani
- Kumbukumbu nzuri
- Uwezo mzuri wa kufikiri na kutatua matatizo

Kwa upande mwingine, njaa na lishe duni husababisha uchovu, usingizi, kutozingatia na kushuka kwa uwezo wa kujifunza. Utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa wanafunzi wanaopata chakula bora shuleni hufanya vizuri kwenye mitihani na masomo kwa ujumla.

## 3. Kupunguza utoro na kuboresha mahudhurio

Programu za lishe shuleni zimeonyesha kuongeza mahudhurio ya wanafunzi, hasa katika maeneo yenye changamoto za kiuchumi. Wazazi wengi hutuma watoto shuleni wakijua kuwa watapata angalau mlo mmoja mzuri kwa siku. Hivyo, lishe shuleni inakuwa motisha ya kuongeza mahudhurio na kupunguza utoro.

## 4. Kuimarisha tabia na nidhamu

Lishe bora inachangia utulivu wa hisia na tabia. Watoto wenye njaa au lishe hafifu wana uwezekano mkubwa wa kuwa na hasira, kuchoka, au kutokuwa watulivu. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliokula vizuri huonyesha tabia njema, ushirikiano, na utayari wa kushiriki katika shughuli za shule.



Picha:MkM

## 5. Kuweka msingi wa tabia bora za ulaji kwa maisha yote

Shule zina nafasi ya kuwafundisha watoto kuhusu umuhimu wa kula vyakula vyenye afya. Kupitia programu za lishe, bustani za shule, na elimu kuhusu vyakula bora, wanafunzi hujengewa misingi ya kufanya maamuzi sahihi kuhusu ulaji hata baada ya kumaliza shule. Hii husaidia kupunguza hatari ya magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari, shinikizo la damu, na unene kupita kiasi wanapokuwa watu wazima.

## 6. Kusaidia usawa wa kijinsia na kijamii

Lishe shuleni husaidia watoto wote bila kujali mazingira yao ya nyumbani. Wanafunzi wanaotoka kwenye familia zenye vipato vya chini hupata fursa ya kula chakula chenye ubora unaofanana na wenzao. Hii inasaidia kupunguza tofauti za kielimu na kijamii zinazoletwa na umaskini.

Lishe shuleni si suala la chakula pekee, bali ni uwekezaji muhimu katika afya, elimu, na mustakabali wa watoto. Shule zinapoweka mkazo kwenye mlo wenye virutubisho sahihi, zinachangia kujenga jamii yenye watu wenye afya bora, wasomi, na wenye uwezo wa kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya taifa. Ni muhimu kwa serikali, wazazi, na walimu kushirikiana kuhakikisha programu za lishe shuleni zinaboreshwa na kuendelezwa.

# Kupitia semina ya mabalozi wa MkM nafanya kilimo ikolojia na kufundisha wengine

***Katika harakati za kusambaza elimu ya kilimo ikolojia kwa wakulima na wadau wa MkM, Mkulima tumefanya ziara ya kuwatembelea wakulima mabalozi na kuona shughuli wanazozifanya kwao na kwa vikundi vya wakulima vinavyohusiana na mchakato mzima wa uzalishaji kwa misingi ya kilimo ikolojia.***

**Suzan Mollel**

Bw. Rajabu Msuya mmoja wa wakulima mabalozi wa MkM kutoka Mwanga (Same) ambaye pia ni mnufaika wa jarida la Mkulima Mbunifu kupitia kikundi chake cha rangaa, ameeleza kuwa amejifunza mengi kupitia makala mbalimbali za jarida la Mkulima Mbunifu lakini zaidi kupitia ziara ya MkM kwa wakulima mabalozi iliyofanyaika Mkoani Morogoro ambayo ilimuongezea hamasa zaidi na kumuongezea nguvu katika kuzalisha kwa misingi ya kilimo ikoljia hasa kwa kufuga kuku, ng'ombe wa maziwa, kilimo cha ndizi, lakini zaidi kuanzisha bustani ya mbogamboga nyumbani kwake.

Nimeweza kufanya shughuli za kilimo na ufugaji kwa ufanisi mkubwa sana, na kwa njia za kitaalamu zaidi kwa muda mfupi toka kuanza kusoma jarida la MkM ambapo alianza kupokea nakala ya kwanza mwaka 2017 mpaka sasa. Aidha, elimu niliyopata katika ziara ya mafunzo imeniwezesha kuanzisha bustani ya mbogamboga nyumbani na najivunia kwani napata mboga salama na za aina mbalimbali kwa mlo mmoja na katika eneo dogo.

## Harakati za kilimo ikolojia

"Nilianza kupata elimu ya uzalishaji kupitia Jimbo la kikatoliki la Same katika mradi wa *Rural farmers intergrated project*, ambao walikuwa wakituletea majarida ya Mkulima Mbunifu lakini pia wakitufundisha njia za uzalishaji kupitia kwa maafisa kilimo wao. Mara tu nilipoanza kufanya kilimo na ufugaji kwa njia ya ikolojia hakika nilianza kuona faida nyingi kubwa hasa ikiwa ni uzalishaji wa chakula salama''.

Aidha, hapo awali nilikutana na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja gharama kubwa za pembejeo hii ikimaanisha mbegu, mbolea na dawa kwa ajili ya wadudu na magonjwa.

Mara baada ya kupata elimu ya kiikolojia nimeweza kujifunza namna ya kufanya kilimo salama na kwa gharama nafuu kwani nimefundishwa njia rahisi na salama za kiasili za kudhibiti magonjwa na wadudu hasa kwa kutengeneza dawa za asili lakini pia kupata mbegu za asili kutoka kwa wakulima wenzangu na kuzalisha kwa ubora zaidi".

''Nimejifunza njia rahisi ya uzalishaji wa mboga salama iliyozalishwa na kukuzwa kwa njia ya asili bila kutumia sumu za viwandani ambazo zina madhara kiafya lakini pia kuzalisha aina nyingi za mboga katika eneo dogo".

## Kwanini Mkulima Mbunifu

Bwana Rajabu anasema kuwa, amepata fursa ya kukutana na wakulima wazoefu katika kilimo ikolojia kutoka mikoa mbalimbali na amejifunza mengi kupitia shuhuda zao lakini pia kazi kwa vitendo hasa pale alipoenda kwenye mafunzo.

Aidha, kupitia elimu aliyopata katika mafunzo, sasa amekuwa mwalimu wa kilimo ikoljia na amefanikiwa kutembelea vikundi vyote vilivyo chini ya usimamizi wake na kuwafundisha namna ya kufanya kilimo cha mbogamboga.

Anaongeza kuwa, kwasasa kila kikundi kina eneo la bustani ya mafunzo yaani shamba darasa, na wanavikundi wameanzisha bustani zao za mboga majumbani kwa ajili ya matumizi ya familia.

''Binafsi nafurahi kuwa kwasasa mke wangu haendi sokoni kununua mboga bali anachuma mboga bustanini na tuna uhakika wa tunachokitumia kuwa ni salama kwa afya zetu.



Picha:MKM




Picha:MkM

Nafurahi pia kuona kuwa, kila aliyenizunguka hata kama hayupo kwenye kikundi, pale anapofika kwangu na kuona shughuli ninazozifanya za uzalishaji kwa misingi ya kilimo hai anapa hamasa ya kutaka kujifunza na hata kufanya kwa vitendo nyumbani kwake" alisema.

## Soko likoje?

Rajabu anasema kuwa soko lipo, na soko la kwanza ni wale waliomzunguka hasa kwa mbogamboga lakini hata kwa mazao mengine kama ndizi na mazao ya mifugo kama kuku, mayai na maziwa yananunuliwa bila shida.

## Changamoto

Bw. Rajabu anasema kuwa, changamoto kubwa ni magonjwa hasa kwa mifugo kama kuku, sungura kwani mara nyingi wanaweza kushambuliwa na magonjwa ya mlipuko lakini pia changamoto kubwa ninayoipata ni kukosa usafiri wa kudumu na wa haraka ambao ungeniwezesha hasa kuwatembelea na kuwafundisha wakulima wengi lakini pia kusafirisha bidhaa au mazao Kwenda kwa wanunuzi''. alisema

## Ushauri kwa wakulima wengine

Bw. Rajabu anatoia rai kwa wakulima ambao hawapati majarida ya MkM kuhakikisha wanapokea na wale wanaopokea kutumia elimu wanayoipata kwenye majarida kwa vitendo zaidi.

***Kwa maelezo zaidi wasiliana na Rajabu Msuya 0759487840.***

# Jarida la MkM limetuwezesha kama kikundi kuzalisha chakula salama

***"Kupitia jarida la Mkulima Mbunifu tumefanikiwa kujifunza namna mbalimbali ya kuzalisha mboga za majani, mahindi, viungo vya chakula kama vile bamia, ngogwe, kuzalisha maboga, pamoja na kutumia dawa za asili kupambana na magonjwa na wadudu ambao mara nyingi ni changamoto katika kilimo wakulima walio wengi na wengi wao huishia kutumia dawa zenye kemikali sumu kutibu tatizo"***

**Abel Lowasa**

Hayo ni maneno ya Bi. Esther Lushino, mkulima na mfugaji, mkazi wa Same visiwani, mkoani Kilimanjaro ambaye ndiyo mkulima balozi wa MkM na msimamizi wa kikundi cha Kimauki chenye wanachama 16.

Mkulima huyu anaeleza kuwa, kilimo na ufugaji ndiyo shughuli kubwa wanayoifanya wakulima wengi same lakini pia wanakikundi wanategemea kilimo na ufugaji kwa ukubwa kulisha na kuendeleza familia zao. Shughuli hizi za kilimo zimeweza kuwaingizia wengi kipato ambayo hutumika katika kumudu gharama na mahitaji yote ya kimaisha.

## Walianzaje kama kikundi

"Sisi tuliungana na kuunda kikundi ambacho kilikuwa na lengo la kuweka na kukopeshana fedha jambo ambalo lilitupa hamasa ya kuendelea kushikamana na ndipo tukaamua kuanzisha bustani za pamoja kulima mazao mbalimbali kibiashara.

Bi. Esther anasema kuwa, kutokana na kuwa hawana maeneo makubwa ya kufanyia uzalishaji, waliamua kuanza kukodi maeneo na kuanza kuzalisha mbogamboga ambazo huuzwa katika masoko ya hapo same.

Aliongeza kuwa, wanalima mazao ya chakula kama vile mahindi, mtama, maharage ambayo hulimwa wakati wa msimu wa mvua na hata kwa njia ya umwagiliaji.

## Mkulima Mbunifu

"Tulianza kupokea na kusoma jarida la Mkulima Mbunifu mwaka 2021 na tulivutiwa sana na elimu iliyopo hivyo tukaendelea kufuatilia na kusoma mara yanapotoka. Aidha, taarifa nyingi za utunzaji wa udongo, kilimo cha mbogamboga, kilimo mesto, utengenezaji na matumizi ya mbolea ya asili, utengenezaji wa dawa za asili kupambana na magonjwa na jinsi ya kutafuta masoko.

Baada ya kusoma tulielewa na tukaanza kuzalisha mbogamboga aina ya sukumawiki, chainizi na mnafu ambapo kwa msimu wote wa mwaka mboga zinapatikana kwa matumizi ya familia lakini pia kwa ajili ya kuuza" aliongeza.

Kupitia jarida hili, tuliweza pia kujifunza na ufugaji wa kuku wa kienyeji kwa lengo la kujiongezea kipato lakini zaidi kupata kitoweo na mayai.

## Mbinu anazotumia katika kilimo

"Kwanza ninazalisha kwa kutumia mbinu za asili au kilimo ikolojia ikiwemo kilimo mesto ambapo huchanganya kahawa, migomba na parachichi, matumizi ya mbolea ya samadi, Pamoja na kilimo cha mzunguko wa mazao".

Kuhusu kudhibiti wadudu na magonjwa, Bi. Esther anaeleza kuwa, anatumia dawa za asili kama mwarobaini, majivu na pilipili.




## Changamoto katika kilimo

Aidha, upatikanaji wa rdhi ya kutosha kulima kwa wingi pamoja na maji wakati mwingine ni changamoto jambo ambalo huweza kupelekea mazao kukauka au kushindwa kufanya uzalishaji.

## Vipi kuhusu wakulima waliowazunguka

Waakulima waliotuzunguka kama kikundi hasa maeneo karibu na shamba darasa wanaanza kuhamasika kutaka kujua tunafanya kilimo hiki na wengi wanahitaji kupata majarida ili kujisomea na kupata elimu kisha kuanza uzalishaji.

## Masoko

Masoko ya mazao ya kilimo ikolojia kwa huku kwetu bado haina tofauti na uuzaji wa mazao yanayozalishwa kwa njia zingine hivyo ni muhimu kuweka mkazo juu ya faida za kilimo ikolojia ili hata wazawa wa ndani waanze kununua lakini pia masoko ya nje yapatikane.

## Wito

"Ninachowashauri wakulima na wafugaji wenzangu, wasiache kusoma jarida la Mkulima Mbunifu na kufanya kile kinachoelekezwa ndani ya jarida hasa kuzalisha mbogamboga kwani ni mazao ya muda mfupi na yanayohitajika nyumbani karibu kila siku''.

***Kwa maelezo zaidi wasiliana na Esther Lushino 0757405329.***



# Kupitia MkM Eva Kyra Anavyowawezesha Wakulima na Wanafunzi

***Eva Kyra ni Mkulima kutoka Babati, Manyara, ambaye amegeuka kuwa sauti muhimu katika kupanua elimu ya kilimo hai na ikolojia.***

**Method Charles**

Safari yake ilianza alipokutana na Jarida la Mkulima Mbunifu kupitia halmashauri na maonyesho ya Nanenane miaka kadhaa iliyopita, jarida ambalo baadaye liliweka msingi wa maarifa yake na kumhamasisha mpaka kufikia kuwa mkufunzi anayewawezesha wakulima na wanafunzi mashuleni kutumia mbinu endelevu za kilimo hai.

Jarida lilibadilisha mtazamo wangu, niliposoma makala mbalimbali ndani ya jarida la Mkulima Mbunifu, niliweza kuelewa mbinu za kilimo hai, namna wakulima wengine walivyofanikiwa, na jinsi walivyotengeneza dawa na mbolea za asili na mbini nyingine nyi za kilimohai. Shuhuda zao ziliingia moja kwa moja moyoni mwangu, nilianza kupata motisha kubwa kuona kuwa inawezekana kulima bila kemikali na bado kupata mazao mengi, bora, na salama.

Nilianza kufanya majaribio shambani kwangu mwenyewe. Nilifuata hatua nilizojifunza kwenye jarida na kuanza kufanya vitu tofauti kama kutengeneza mbolea za asili, kutengeneza dawa za asili za mimea, na kutumia mbinu rafiki kwa mazingira. Kadri nilivyoendelea, niliona tofauti kubwa kwenye mimea, udongo, na hata afya ya familia yangu.

Matokeo Shambani kwangu, leo hii shamba langu linaendeshwa kwa kanuni za kilimo hai pekee. Natumia mbolea za asili, dawa za asili, na mbinu hii ya Super Grow ninayoitengeneza mwenyewe kwa kutumia:

- Majani mabichi ya miti mbalimbali
- Mazapreshi (mabaki ya mimea)
- Molases lita 4
- Maji lita 80–100
- Mifupa ya ng'ombe, maganda ya ndizi na maembe
- Majivu
- Mchanganyiko maalum wa kufanyia uchachishaji

Kupitia mchanganyiko huu, mimea yangu inapata virutubisho vya kutosha, inakua haraka, inakomaa vizuri, na inastahimili magonjwa. Ninalima mbogamboga kama vile mchicha, spinachi, sukuma wiki, nyanya na bamia n.k. ninawateja wengi kwa sababu wateja wangu wanajua hazina kemikali.


Picha:MkM

### Faida kwangu na familia kupitia kilimo hai:

- Nimepunguza gharama za pembejeo
- Nimeboresha afya ya familia kwa kula chakula salama
- Nimepata kipato cha kutosha na cha uhakika
- Nimeongeza uzalishaji bila kuharibu udongo wangu shambani

Haya yote yalianza kupitia elimu niliyoipata kwenye jarida la Mkulima Mbunifu.

Safari ya fuwafundisha Wakulima wenzangu, ni baada ya kuona mafanikio yangu, nilihisi kuwa si haki kukaa kimya. nilitamani elimu hii iwafikie wakulima wengi zaidi. Nilianza kufundisha:

- Vikundi vya wakulima
- Mtu mmoja mmoja
- Shule za msingi kupitia elimu ya ikolojia

Watuwengi wana niuliza kwa nini nimejikita sana kufundisha


Picha:MkM

mashuleni elimu hii ya kilimo hai na kilimo ikolojia? Ni kwasababu Watoto wanajifunza haraka. Wanapofika nyumbani huwasimulia wazazi, hivyo elimu inasambaa upesi. Pia tunalinda afya ya watoto na kuimarisha lishe yao kupitia bustani za shule.

Ninapokutana na mkulima ambaye amekataa kuanza kilimo hai huwa simwachi, ninacho kifanya huwa niarudia rudia maranyi hadi wengi wao huwa wanaanza kuamini na kujaribu. Kingine ninacho kifanya ninafanya kwa vitendo kwa kutengeneza bustani za majaribio na dawa za asili ziwe mfano halisi wa kuwashawishi kuanza kufanya kilimo hai.

Ujumbe wangu kwa Wakulima wenzangu, Leo dunia napambana na magonjwa mengi yanayoanzia kwenye chakula. Kama mkulima unaweza kuyalinda mashamba yako na familia yako kupitia kilimo hai.

Jarida la Mkulima Mbunifu limekuwa mwongozo mkubwa kwangu na kwa yeyote ambaye ana lipata lakini halisomi, anakosa hazina ya elimu. Ndani yake kuna mbinu za kilimo hai, ufugaji, utengenezaji wa mbolea na dawa za asili kwa mimea, ujasiriamali na mifano halisi ya wakulima waliobadilisha maisha yao kupitia kilimo ikolojia na kilimo hai.

***Kwa maelezo zaidi wasiliana na Eva Kyara kwa simu namba 0784 733968.***

# Kupitia Mkulima Mbunifu nimeweza kufundisha wengine kilimo ikolojia

***''Naitwa Thomas Amas Kondeya, ni mkulima balozi wa Mkulima Mbunifu toka Singida (Ikungi. Ninajishughulisha na uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa misingi ya kilimo mara baada ya kupata elimu kupitia Mkulima Mbunifu pamoja na vipindi vya kilimo ikolojia toka Farm Radio kupitia kituo cha radio cha Standard FM''.***

**Dorothea Chambo**

Hivyo ndivyo alivyoanza kujieleza Bw. Thomas Kondeya ambaye kwa ujumla alianza shughuli za uzalishaji mara tu alipohitimu elimu yake ya msingi kwa kuzalisha mahindi ya asili, mtama, uwele pamoja na alizeti.

Bwana Thomas anasema kuwa, alifanya uzalisha wa mazao mpaka mwaka 2021 alipopata elimu ya kilimo ikolojia ndipo alipoamua kuachana na kilimo cha zamani cha mazoea na kujikita moja kwa moja kwenye kilimo ikolojia.

''Wakulima wengi wanazalisha kwa kilimo cha kawaida cha mazoea bila kutumia mbinu za kilimo ikolojia kujiongezea uzalishaji na kufanya kilimo cha tija'' alisema.

## Mkulima Mbunifu

Nilianza kupokea jarida la Mkulima Mbunifu, mwaka 2024, ambapo nakala za jarida hili nilipata kutipia Farm Radio walipokuwa wakifanya ziara zao za kutembelea vikundi vya wakulima wanaonufaika na mdari wa kilimo ikolojia kupitia vipindi vya radio.

Thomas anaeleza kuwa, aliweza pia kutembelewa na Erica Rugabandana meneja wa mradi wa Mkulima Mbunifu na kuweza kumueleza kwa undani kuhusu jarida la Mkulima Mbunifu na nini wanafanya kwa wakulima.

Kupitia jarida hili nimeweza kujifunza mambo mengi mazuri na kuanza kupata mafanikio baada ya utekelezaji wa yale yaliyoandikwa.

- Nimeweza kujifunza kutumia mbolea za mboji, samadi, kufukia mabaki ya mazao kwa lengo la kurutubisha udongo jambo ambalo nimeona mafanikio makubwa kwatika uzalishaji.
- Nimeweza kuboresha shamba kwa kurutubisha yaani kwa kuchoma mabua ya mabaki ya mazao kwa ajili ya kuotesha mazao ambapo mabaki haya yaliyochomwa husaidia kuhifadhi maji wakati wa ukame.
- Nilifanikiwa pia kuanza kufanya kilimo cha mbogamboga kwa kutengeneza bustani ya nyumbani lakini pia nikajifunza kutengeneza dawa za asili zinazoweza kusaidia kuua wadudu na magonjwa ya mbogamboga.
- Nilifanikiwa kuanzisha kikundi cha watu 7, wanawake wanne na wanaume watatu kupitia farm radio na Mkulima Mbunifu lakini kuanzia mwaka 2024 nilifanikiwa kuunda vikundi vingine 12 hivyo kwa ujumla ninahudumia vikundi 13 pamoja na shule za msingi 3 ambapo nawafundisha mbinu mbalimbali za uzalishaji kwa misingi ya kilimo ikolojia hasa kuanzisha bustani za mbogamboga.
- Napokea na kusambaza majarida ya Mkulima Mbunifu na kuhamasisha wakulima kusoma na kufanya kwa vitendo zaidi.



Picha:MkM

## Changamoto kwenye kilimo hai

- Changamoto kubwa ni wakulima kuwa na kilimo cha mazoea yaani kutumia mbolea za kemikali sumu za viwandani pamoja kutumia mbegu chotara.
- Linapokuja swala la utekelezaji, wakati mwingine huweza kuwa mgumu mara tunapokutana na maafisa kilimo ambao huona kama sisi wa kilimo ikolojia tunawakosesha wateja wao, jambo ambalo huweza likatukosanisha na serikali.

Mkulima Mbunifu kusisitiza mbegu za asili na mbolea na watu kuanza kufikiria na kutumia mbegu za asili. Watu 110 tayari wameanza kutekeleza uoteshaji wa kilimo hai.

## Wito

Natoa ombia kwa Mkulima Mbunifu kuendelea kutufuatilia kwa ukaribu zaidi yaani kufanya ziara ya mara kwa mara ili kuweza kutambua tulikotoka na tunakoenda na namna tutakavyoweza kufika na kuondokana na vizuizi au changamoto za uzalishaji.

Mkulima Mbunifu ifanye utambulisho katika halmashauri, ofisi za kata na za Kijiji ili kuweza kuwasaidia maafisa kilimo kutambua zaidi nini tunafanya na pia kuwezesha shughuli zetu Kwenda sawia.

***Kwa maelezo zaidi wasiliana na Thomas Amas 0748308820.***


Picha:MkM

# Maoni na maswali toka kwa wasomaji wa makala za Mkulima Mbunifu

***Ili kufikia malengo katika uzalishaji ni lazima kutafuta taarifa sahihi kuhusu mradi wako na kutokusita kuuliza maswali pale unapokwama ili kupata utatuzi wa changamoto yako.***

**MkM**

Hawa ni baadhi ya wasomaji wa makala mbalimbali za Mkulima Mbunifu ambao wameendelea kufuatilia pamoja na kuuliza maswali na kupata ushauri toka Mkulima Mbunifu. Tutumie swali lako nasi tutakujibu:

**Jesca Ryatura** anauliza; Ng'ombe wangu aliindia joto saa kumi jione akapandishwa siku ya pili saa 4 asubuhi, baada ya siku moja akatoka damu ukeni. Je, ng'ombe huyo atakuwa ameshika mimba au ana tatizi kwenye mfumo wa uzazi?

Mkulima Mbunifu; Unapoona damu inamaanisha kuwa umeshamchelewesha ng'ombe kupata dume na inaonyesha kuwa ng'ombe wako alikua kwenye joto siku 3 zilizopita. Itabidi ungoje mpaka siku 18-22 zijazo za joto kabla ya kufanya uhamilishaji.




**Dezidery Pamphily** anauliza; Hivi unaweza kuwalisha ng'ombe chakula tu cha ziada bila kuwapa nyasi

Mkulima Mbunifu; Habari, Karibu Mkulima Mbunifu na asante kwa swali lako.

Vyakula vya ziada haiwezi kutosheleza uhitaji wa chakula cha ng'ombe. Chakula cha ziada ni kama vile mchanganyiko wa aina mbalimbali za pumba na vitamini vingine au madini muhimu kama chumvi, kwa maana hiyo, ng'ombe ni lazima alishwa majani iwe nyasi au aina nyingine yeyote ya majani lakini chakula cha zaida pekee hakiwezi kuwa mlo unaweza kumtosheleza ng'ombe.




**Bright** anauliza; Je, ndama anapaswa kuachishwa maziwa akiwa na umri gani na kama kwa bahati mbaya amekunywa maziwa mengi ni hatua gani ichukuliwe kumsaidia?

Mkulima Mbunifu; Habari, Karibu Mkulima Mbunifu na asante kwa swali lako. Ndama huachishwa maziwa akiwa na umri kati ya miezi mitatu au minne na akiwa alilishwa vizuri wakati wote toka kuzaliwa.

Iwapo ndama ataanza kuharisha, acha mara moja kumnywesha maziwa mpaka pale atakapopona.

Badala ya kumnywesha ndama maziwa, mnyweshe maji safi na salama yenye uvuguvugu na ikiwezekana weka chumvi kidogo au glucose.

Hakikisha maji unayomnywesha ndama kwa wakati huo ni ya kutosha kwani maji ni muhimu sana kutokana na ukweli kuwa kinachosababisha kifo cha ndama wakati wa kuharisha ni kukosekana kwa maji mwilini.




Kama imethibitishwa kuwa kinachomfanya ndama kuharisha si unyweshaji wa maziwa mengi kupita kiasi basi apewe dawa za viua bakteria yaani antibiotic.

Wafunze ndama kula vyakula na malisho makavu wakiwa na umri wa majuma mawili ili kuwasaidia wasiharishe. Unaweza kumpa vyakula vya kusindika kwenye mdomo au kuweka kidogo kwenye ndoo au chombo mara tu anapomaliza kunywa maziwa kwenye chombo hicho.

**Charles Ilago Milamo** anauliza; Ikiwa ndama anaharisha na umeamua kumpa maji safi na salama na chumvi inatosha bila kumpa maziwa tena akawa anatumia maji tu.

Mkulima Mbunifu; Habari, Karibu Mkulima Mbunifu na asante kwa kuendelea kufuatilia na kusoma




makala mbalimbali za jarida hili. Ikiwa ndama anaharisha kunakotokana na unyweshaji wa maziwa acha kumnywesha maziwa mara moja na endelea kumpa maji mengi safi na salama mpaka hapo atakapopona na utaendelea kumnywesha maziwa lakini pia ni muhimu kumpatia antibiotiki. Na kama ndama hajaanza kula majani hakikisha unamuanzisha kula kidogokidogo mara tu anapofikisha wiki mbili hii itamsaidia kupata majanikiasi na maziwa kiasi na kumpunguzia nafasi ya kuweza kuharisha kunakotokana na maziwa.



Haki zote zimehifadhiwa ©2025 *Mkulima Mbunifu*